035713655

**KENYA NATIONAL PREDICTION TESTS**

# KCPE

516004

# KISWAHILI
# SEHEMU YA KWANZA
# LUGHA

**Muda: Saa 1 dakika 40**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**
**SOMA MAAGIZO YAFUATAYO KWA MAKINI.**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida.
4. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

5. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
6. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
7. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
8. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
9. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

   **Mfano:**

   **Katika kijitabu cha maswali:**

   **22.** Barua ya kuomba kazi huitwa
   A. waraka
   B. barua maalum
   C. barua ya kiofisi
   D. Barua rasmi

   Jibu sahihi ni **D**

   **Katika karatasi ya majibu:**

   **2.** [A] [B] [C] [D] **12.** [A] [B] [C] [D] **22.** [A] [B] [C] [D] **32.** [A] [B] [C] [D] **42.** [A] [B] [C] [D]

   Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **22**, kisanduku chenye herufi **D** ndicho kilichochorwa kistari.

10. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
11. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa.**

906504

© *Mtihani Bora*

**GEUZA UKURASA**

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 hadi 15. Katika kila nasi, umepewa viteuzi vinne, chagua kifaacho zaidi kuujazia mwanya.***

Mashairi yaliyo na ubeti mmoja yaani ____1____ pia hutungwa na _____2____. ____3____ anaweza kuyaimba katika tamasha ____4____. Ninawajua watu wengi ambao ____5____ ushairi umewawia nia mwafaka ya kuzumbua ____6____. Ile dhana kwamba mtu _____7_____ Kusoma ama maisha yake yataharibika, sasa imewatoka wengi wakaanza kuona kuwa, hata ____8____ ____9_____ mtu, akiitumia vizuri, inaweza kuwa njia bora ya ____10____ pesa.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. tathmina | B. thathnia | C. utenzi | D. tasmina |
| 2. | A. malenga | B. manju | C. mshairi | D. ngoi |
| 3. | A. Mkariri | B. Hatibu | C. Mhasibu | D. Mghani |
| 4. | A. anapofunza | B. lolote | C. anayefunza | D. afunzapo |
| 5. | A. sanii hii ya | B. usanii hii ya | C. usanii huu wa | D. Sanaa huu ya |
| 6. | A. chakula | B. chajio | C. staftahi | D. riziki |
| 7. | A. anashurutika | B. halazimiki | C. ana budi | D. hashurutiki |
| 8. | A. kipaji | B. karama | C. karima | D. zawadi |
| 9. | A. uliyo nayo | B. akiwa nayo | C. aliyo nayo | D. ukiwa nayo |
| 10. | A. kutafutia | B. kuzalishiwa | C. kutafutiwa | D. kuzalisha |

Nilikuwa nimeketi kwenye ___11____ huku nikimsubiri aliyekuwamo ___12____ ndipo nikamwone daktari anieleze ____13____. Hazikupita ____14____ kabla ya kusikia jina langu ____15____.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 11. | A. majilisi | B. pambajio | C. ofisi | D. chumba |
| 12. | A. afike | B. awasili | C. aingie | D. atoke |
| 13. | A. kilichoniuguza | B. mwake | C. wake | D. pake |
| 14. | A. siku nyingi | B. masaa mengi | C. dakika nyingi | D. saa mingi |
| 15. | A. akiita | B. akiniita | C. nikiitwa | D. likiitwa |

***Kuanzia swali la 16 hadi 30, chagua jibu sahihi katika kila swali.***

16. Teua kati ya hizi, sentensi ambayo ina kiwakilishi cha pekee.
   A. Wengi wape ama watajichukulia peke yao
   B. Ambaye analitaka tunda hili aje alichukue
   C. Wenye magari haya hawayajapakia vizuri
   D. Baadhi ya wanaoniita ni marafiki zangu

17. Ni sentensi gani iliyo sahihi kisarufi?
   A. Wanatoka katika nchi geni
   B. Rinda lake zee litatupwa
   C. Utakula tunda mbivu ama mbichi?
   D. Rangi jekundu la bendera yetu ni ishara ya damu

18. Chagua sentensi iliyotumia kiambishi **-po-** kuonyesha masharti
   A. Mlimani palipojengwa nyumba pananyesha mvua
   B. Nipokuwa na haja ya kumwona, ninaenda kwake
   C. Usipotahadhari utajikuta hatarini
   D. Kila tuendapo mashambani tunafurahi kukaa na nyanya

19. Chagua ulinganisho sahihi
   A. Mkutubi hutoa hotuba mikutanoni
   B. Hatibu hutunza vitabu maktabani
   C. Katibu hupanga vitabu kwenye maktaba
   D. Karani wa korti huandika mambo yanavyoendelea kortini

20. Badili sentensi ifuatayo katika usemi taarifa.
**"Mambo ambayo baba ameyasema leo yamenivunja moyo." Abdul alisema.**
   A. Abdul alisema kuwa mambo aliyoyasema baba yake leo yalimvunja moyo
   B. Abdul alisema kuwa mambo aliyoyasema baba yake siku hiyo yalimvunja moyo
   C. Abdul alisema kuwa baba, mambo ambayo uliyasema silu hii yamenivunja moyo
   D. Abdul alisema kwamba siku hiyo mambo ambayo ameyasema baba yamemvunja moyo

21. Ukanusho sawa wa sentensi:
**Mwanafunzi anayetii anachoambiwa amefanikiwa maishani.**
   A. Mwanafunzi anayetii anachoambiwa hajafanikiwa maishani.
   B. Mwanafunzi asiyetii anachoambiwa hatafanikiwa maishani.
   C. Mwanafunzi asiyetii asichoambiwa hajafanikiwa maishani.
   D. Mwanafunzi anayetii anachoambiwa hatafanikiwa maishani.

22. Shada na koja ni kwa maua kama vile ______ na ______ ni kwa ndizi
   A. Kikonyo na mkungu
   B. Mkunga na chane
   C. Mkungu na chane
   D. Kikuba na fungu

23. Mzazi mwenye tabia ya kumtetea mwanawe hata wakati ambao amefanya makosa anafaa kupewa nasaha kwa methali gani kati ya hizi?
   A. Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu
   B. Mwana mtukana nyina, kuzimuni enda kiona
   C. Mchelea mwana kulia hulia yeye
   D. Asiyesikia la mkuu hupatwa na makuu

24. Chagua kundi linaloonyesha nomino isiyotokana na kitenzi kwea
   A. ukwezi
   B. kukwea
   C. kweza
   D. mkwezi

25. Kauli sahihi miongoni mwa hizi ni kwamba
   A. Kivumishi kinaweza kueleza kuhusu kiwakilishi cha nomino
   B. Kitenzi hakiwezi kubadilika kikawa nomino
   C. Kiashiria na kimilikishi ni maneno yenye maana sawa
   D. Kielezi hutumika kuonyesha hisia katika sentensi

26. Onyesha ni katika sentensi ipi ambapo kiambishi "**-ji-** "kimetumika kuonyesha utendaji?
   A. Inaaminika kwamba wauzaji wengi wameenda hasara
   B. Ujuaji wako utakutia hatarini mwenzangu
   C. Jibwa lililobweka liliashiria hatari katika makazi yetu
   D. kwa nini wajiongelesha kama mwehu?

27. Ni nani kati ya wasichana hawa hakutoa maelezo sahihi kuhusu majina ya uhusiano?
   A. Mpwa ni mtoto wa dada au kaka yangu
   B. Mkoi ni mtoto wa shangazi yangu
   C. Binamu ni mtoto wa halati yangu
   D. Wifi ni mke wa mjomba wangu

28. Ni lipi kati ya maneno haya ni nomino fungamano?
   A. kusakura
   B. weusi
   C. maziwa
   D. upepo

29. Badili sentensi hii katika hali ya wingi.
   **Jogoo wa shamba hawiki mjini**
   A. Jogoo wa shamba hawawiki mjini
   B. Jogoo wa mashamba hawawiki mijini
   C. Majogoo wa mashamba hawawiki mijini
   D. Majogoo wa mashamba hawawiki mjini

30. Ni wapi ambapo pametumia maamkizi ya kutakiana heri na amani?
   A. Cheichei nyote mliofika hapa leo hii?
   B. Nawasabahi kaka na madada zangu
   C. Sabalkheri mabibi na mabwana?
   D. Salaam aleikum ndugu zangu wapendwa?

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 - 40.***

Matokeo ya mtihani yalipotangazwa, Khalif alikuwa miongoni mwa wanafunzi kumi bora waliokwangura alama za juu katika kaunti yake. Alama mia tatu sitini na saba! Akaitwa katika shule ya kitaifa jijini Jua. Akajawa na furaha iliyotishia kumtia wazimu. Mungu kamtembelea katika shule yake kule kijijini na kumteua atoke mashambani angalau aone ukuu wa jiji kuu! Kama si kwa neema ya msomi mmoja tajiri jirani, walahi asingeweza kuona hata lango la shule ile, wacha kuingia ndani.

Yule bwanamdogo hatimaye akaingia jijini akiwa kuku mgeni kabisa! Tujuavyo, kuku mgeni hakosi kamba mguuni. Hakujua hata kuunganisha mawasiliano katika lugha ya kimombo! Kiswahili chenyewe kilikuwa kile cha kuokotaokota tu, tena kilichoathiriwa vilivyo la **lafudhi**. Badala ya kusema "sipendi mchezo," alijikuta akiwaambia waliomchezea, "mimi bana benda mucheso!" Akashangaza hata zaidi huku wenzake waliotoka miji mingine mikubwamikubwa wakishangaa aliokotwa kutoka uchochoro upi! Alifukuliwa kutoka shimo gani! Mtihani nao ulipofika, Khalif aliona soni kujikuta huko, zaidi ya nambari mia saba na nne kwa mia saba na watano! Yaani kwa wawili bora kutoka kule mwisho, alijinyakulia nafasi ya pili!

Aibu ilimpiga pambaja, juu ya ushamba akaongeza upumbavu. Hajui hili wala lile. Kwa nini aendelee kukaa katika shule itakayomsukuma kaburini mapema? Ule uchu aliokuwa nao wa kusomea katika shule nzuri ukaisha kama bonge la barafu lililoyeyushwa na tanuri. Katika likizo ya kwanza, Khalif alimweleza mama yake kuwa asingetamani kurejea katika shule ile kwani ubaya wake ulizidi uzuri. Wazazi hawakumsikiliza wala kumwonyesha huruma. Wao ndio waliompigia mwalimu simu, wakitaka kujua maendeleo ya Khalif shuleni, naye akawaambia waziwazi kwamba alihitaji usaidizi kujielewa ndipo aanze kuyaelewa masomo. Akawauliza kama walikuwa na habari kwamba Khalif hujiona hafai kitu na kuishia kujidharau.

"Hilo linawezekana mwalimu kwa sababu ya mazingira aliyozaliwa na kukulia. Hapa tulipo dunia bado imo usingizini wala haijafungua hata jicho moja. Yeye ndiye tunayemsubiria aje kutuwashia taa." Walikiri wazazi wa Khalif huku wakiahidi kumpiga jeki na kumpa ushauri wowote ambao angeuhitaji ili kuyathamini upya masomo yake hata kuliko alivyofanya awali. Hili walifanya kwa kumtafuta mshauri nasaha wa kielimu. Walimpeleka Khalif kwake naye akamchambua taratibu kama karanga hadi akatambua kwamba kikuu kilichomsumbua kuliko chochote ni kujilinganisha na wenzake. Wenzake ambao hakuelewa asili wala fasili yao. Mshauri akamfunza kwamba katika dunia hii tunayoishi, mambo ni kama vidole na hayakosi kuzidiana.

"Daima dawamu, watakuwapo watu katika maisha yako wanaokuzidi kimaisha na unaowazidi kimaisha. Aliko mtu sasa, siko alikokuwa jana. Nawe uliko leo, siko utakakokuwa kesho. Ila hilo linategemea jinsi unavyoitumia leo yako. Ukiichezea, kesho utazama hata chini zaidi. Ama hujasikia usemi wa wahenga kwamba ukicheza ujanani utalipa uzeeni? Ungependa kuwa mwanabiashara mahiri kesho? Anza sasa kupiga hesabu zako. Lakini ukitaka kuwa mkata aliyekatwakwatwa na ukata pande zote, kaa hapo uendelee kujionea huruma. Kesho yako ipo mikononi pako. Uko huru kuiunda au kuibomoa. Chagua!" Busara ya mshauri nasaha ilimfumbua Khalif macho, akaamua kurejea shuleni na mtazamo chanya akayatoe jasho yale majabali ya masomo kwani, penye nia hapakosi njia.

31. Kwa mujibu wa aya ya kwanza
   A. wazazi wa Khalif walimwomba tajiri mmoja amlipie karo
   B. alama alizopata zilimfanya Khalif kumtafuta mdhamini
   C. Khalif alikuwa mwanafunzi bora zaidi nchini mtihanini
   D. si Khalif aliyeibuka mwanafunzi bora katika mtihani huo taifani

32. **Lafudhi** kama lilivyotumika katika kifungu ni
   A. Kukosa uwezo wa kuwasiliana katika lugha ya taifa
   B. Kuokotaokota na kutumia maneno ya lugha nyingine
   C. athari ya lughamama katika maongezi ya mtu
   D. Matumizi mabaya ya sarufi katika lugha nyingine

33. *"Ule uchu aliokuwa nao wa kusomea katika shule nzuri ukaisha kama bonge la barafu lililoyeyushwa na tanuri."* Hapa mwandishi ametumia tamadhali gani ya lugha?
   A. Tashihisi
   B. Tashbihi
   C. Sitiari
   D. Msemo

34. Kwa nini Khalif alilemewa kimasomo?
   A. Walimu hawakujua kufunza vyema ipasavyo
   B. Hakuwa mwanafunzi bora zaidi kwa hivyo kushindwa kungetarajiwa
   C. Alijiunga na marafiki waliompotosha na kumpotezea wakati
   D. Wanafunzi wenzake hawakutaka kuhusiana naye shuleni

35. Ni mambo yapi mawili yaliyomfanya Khalif kutamauka masomoni shuleni kwake?
   A. Alama duni na kukosa kulipiwa karo
   B. Kuchokozwa na wenzake na umbali wa shule
   C. Mafunzo duni na kuchokozwa na wenzake
   D. Matokeo duni na kufanyiwa stihizai na wenzake

36. Kabla ya kuwasiliana na mwalimu
   A. mwalimu hakumwona Khalif kuwa na tatizo lolote.
   B. wazazi walimwonya Khalif kuwa wangepiga simu shuleni
   C. Khalif hakuwa na haja ya kuwaelezea wazazi alama alizopata
   D. wazazi hawakujua kabisa kilichomtatiza mwanao

37. Changamoto kuu ya Khalif ilikuwa
   A. wanafunzi waliomtenga nao
   B. alama zake masomoni
   C. mazingira aliyokulia
   D. utovu wa nidhamu

38. Hatari ambayo ingetokea iwapo Khalif asingeyakamilisha masomo ni kwamba
   A. aliyemlipia karo angevunjika moyo na kukataa kusaidia wengine
   B. eneo aliloishi lisingepata mtu wa kuwaletea mwanga
   C. wazazi wake wasingeweza kumlipia karo kwingine
   D. angefukuzwa shuleni na hatimaye nyumbani

39. Mshauri wa Khalif alikuwa na nia gani katika ushauri wake?
   A. Kumdhihirishia Khalif tofauti zilizo maishani na manufaa ya kujitahidi
   B. Kumweleza Khalifu jinsi ya kuwashinda walio mbele yake maishani
   C. Kuwasaidia wazazi wa Khalif kubadilisha mienendo yake mibaya
   D. Kumwelekeza Khalif ajue njia ya kuchukua nafasi bora masomoni

40. Kifungu kinakamilika
   A. Wazazi wa Khalif wakiwa wametamaushwa na mwanao
   B. Kwa njia chanya ambapo mambo yanatarajiwa kuwa sawa
   C. Khalif akiwa ameghadhabishwa kwa kuambiwa ajichagulie maisha
   D. Matokeo ya Khalif yakiwa yameimarika sana darasani

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 – 50.***

Twaja na furaha ghaya, tukiwa wenye buheri,
Ndio leo twajimwaya, kuwaletea habari,
Hatuneni kwa ubaya, twawaeleza mazuri,
Shule yetu shule bora, shule ya kujivunia.

Tangu tisini na tatu, shule ilipoanzishwa,
Miaka kumi na tatu, ya watoto kufundishwa,
Ni bidii kila mtu, hakuna kushurutishwa,
Shule yetu shule bora, shule ya kujivunia.

Kila mwaka nenda rudi, wanafunzi wanolewa,
Kila mtu hana budi, kila jambo kuelewa,
Vijana wajitahidi, kwa lile **wasilojuwa**,
Shule yetu shule bora, shule ya kujivunia.

Wako wapi walohema, kukimbia kwenda mbele
Sasa hivi wako nyuma, wakiwa na wivu tele,
Sisi twapanda mlima, tufike chake kilele,
Shule yetu shule bora, shule ya kujivunia.

Kila mwaka mikakati, mipango kujiundia,
Mizaha hapa hupati, bidii sote twatia,
Ukitaka ithibati, matokeo angalia,
Shule yetu shule bora, shule ya kujivunia,

Michezoni twabobea, pia hatuachwi nyuma,
Kazini twajitolea, kufundishwa mengi mema,
Mengi ya kujivunia, hata kompyuta twasoma,
shule yetu shule bora, shule ya kujivunia.

Tumefika ukingoni, tumewapasha habari,
Kwa wazazi **shukurani**, kutuleta shule nzuri,
Tuna furaha nyoyoni, tunazidi kunawiri,
Shule yetu shule nzuri, shule ya kujivunia.

41. Kwa jumla, shairi halijazungumzia
   A. wanafunzi wanavyosoma kwa juhudi kwa hiari yao
   B. udadisi wa wanafunzi katika mambo wasiyoyaelewa rahisi
   C. afya ya wanafunzi katika shule hiyo tajika
   D. utepetevu wa walimu unaotishia kuzua matokeo duni

42. Katika ushairi, ni kauli gani sahihi?
   A. Kipande cha tatu cha mshororo huitwa ukwapi
   B. Ili kupata vina vya kati na vya mwisho, lazima mizani yote ilingane
   C. Mwandamizi ni mstari unaoandamana na kibwagizo katika ubeti
   D. Mshororo wa tatu wa ubeti huitwa mleo

43. Kufikia mwaka wa elfu mbili ishirini na mbili, shule inayozungumziwa
   A. inategemewa kuwa miongoni mwa shule bora nchini
   B. itakuwa imeongezeka kimaendeleo na kimatokeo
   C. itakuwa imedumu miaka karibu ishirini na tisa
   D. itadumisha wanafunzi, matokeo na maendeleo

44. Maneno, wasilojuwa na shukurani yamekolezwa rangi. Yamehusisha mbinu gani ya ushairi?
   A. utani
   B. mazida
   C. majazi
   D. inkisari

45. Kwa mujibu wa ubeti wa tano
   A. hakuna anayezembea katika masomo baina ya walimu na wanafunzi
   B. matokeo mema yamewafanya waliowatangulia kujifunza jambo
   C. umechangiwa na ushirikiano wa walimu, wazazi na wanafunzi
   D. ubora wa shule kimasomo unadhihirika katika alama nzuri mtihanini

46. Chagua methali inayoingiana sawa na ubeti wa nne
   A. Safari ya kesho hupangwa leo
   B. Kutangulia si kufika
   C. Mwangata mbili moja humponyoka
   D. Bidii huleta ufanisi

47. Shairi hili ni aina mojawapo ya
   A. utenzi
   B. majibizano
   C. ngonjera
   D. unne

48. Chagua kauli katika shairi inayoonyesha tashihisi
   A. Tumefika ukingoni, tumewapasha habari
   B. Mengi ya kujivunia, hata kompyuta twasoma
   C. Kila mwaka nenda rudi, wanafunzi wanolewa
   D. Shule yetu shule nzuri, shule ya kujivunia

49. Shairi ulilolisoma halina
   A. mwandamizi
   B. kituo
   C. mwelekeo
   D. msisimko wowote

50. Katika shairi kuanzia mwanzo hadi mwisho, mwandishi
   A. anaangazia changamoto anazopitia shuleni
   B. anasifia ubora wa shule anayosomea
   C. anaonyesha bidii na uwajibikaji wa walimu
   D. anazungumzia jinsi ya kufanya watu wajue matokeo ya shule

**Andika insha ya kusisimua isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukumalizia kwa maneno yafuatayo:**

.......... Kila nilipoangalia mafanikio yangu, nilielewa kweli kuwa shida hazidumu, na hakuna aliyeumbiwa shida duniani humu.